Jamhuri ya Muungano wa Tanzania

# MAELEZO YA MSINGI YA SENSA YA WATU NA MAKAZI 2012

Ofisi ya Taifa ya Takwimu
Wizara ya Fedha
Dar es Salaam.

Ofisi ya Mtakwimu Mkuu
Serikali ya Mapinduzi
Zanzibar

Januari, 2012

# Yaliyomo

Ukurasa

Dibaji ........................................ iii
1. Utangulizi ........................................ 1
2. Maana ya Sensa ya Watu na Makazi ... 2
3. Sensa na Maendeleo ........................ 4
4. Umuhimu wa Sensa ya Watu na Makazi ya Mwaka 2012 .................... 5
5. Maandalizi ya Sensa ya Watu na Makazi ya Mwaka 2012 .................... 6
   5.1. Kutenga Maeneo ya Kuhesabia Watu ........................................ 7
   5.2. Uhamasishaji ............................ 9
   5.3. Sensa ya Majaribio .................... 10
   5.4. Maandalizi Mengine .................. 13
6. Kamati za Sensa ............................... 13
7. Wajibu wa Viongozi ........................... 14
8. Wajibu wa Wananchi ......................... 18
9. Maswali ya Sensa .............................. 19

10. Sheria ya Takwimu na Usiri wa
Taarifa za Wanakaya ........................ 24
11. Maeneo Maalum ya Kuhesabu Watu . 25
12. Wawindaji, Wavuvi naWachungaji ..... 26
13. Wasafiri ........................................ 27
14. Watu Wasiokuwa na Makazi
Maalum ......................................... 29
15. Siku ya Sensa ................................. 30
16. Muda wa Kuhesabu ........................ 30

# Dibaji

Maelezo haya ya msingi kuhusu Sensa ya watu na makazi ya 2012 yametayarishwa na Ofisi ya Taifa ya Takwimu ikishirikiana na Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, ambazo ndizo zenye jukumu la kufanya Sensa ya Watu na Makazi ya mwaka 2012. Shabaha kuu ya Maelezo haya ni kumuelimisha kwa kumpatia kiongozi taarifa muhimu juu ya Sensa, ambazo atazitumia katika shughuli za uhamasishaji.

Taarifa hizo ni pamoja na kujua Sensa inafanyika lini, vipi na kwa nini inafanyika, kwa nini ni muhimu wananchi na wadau wengine kushiriki katika kufanikisha Sensa. Kitabu kimefafanua wajibu na umuhimu wa wananchi, viongozi pamoja na wadau mbalimbali kushiriki kikamilifu katika kuchangia juhudi za kufanikisha maandalizi ya Sensa na Sensa yenyewe.

Masuala mbalimbali ya Sensa ya Watu na Makazi ya mwaka 2012 yamefafanuliwa kwa kifupi. Ni matumaini yetu kuwa matumizi mazuri ya kitabu hiki wakati wa uhamasishaji yatasadia kuepusha utoaji wa taarifa/ujumbe tofauti kwa wananchi juu ya Sensa.

Tunawaomba viongozi wote washirikiane nasi katika kueneza ujumbe huu kwa wananchi. Aidha, Maafisa wetu walioko wilayani wataendelea kufafanua zaidi ili kutoa elimu kwa wote.

Dkt. Albina A. Chuwa,
Mkurugenzi Mkuu
Ofisi ya Taifa ya
Takwimu
Dar es Salaam.

Mohamed Hafidh Rajab,
Mtakwimu Mkuu
Ofisi ya Mtakwimu Mkuu
Serikali ya Mapinduzi
Zanzibar.

**Januari, 2012**

# 1. Utangulizi

Mwaka 2012 ni mwaka wa Sensa ya Watu na Makazi nchini. Sensa itafanyika tarehe 26 Agosti 2012 miaka kumi baada ya Sensa ya mwisho iliyofanyika mwaka 2002. Hii itakuwa Sensa ya tano kufanyika tangu Tanzania kupata uhuru. Sensa zilizotangulia zilifanyika katika miaka ya 1967, 1978, 1988 na 2002.

Ili kupata ushirikiano mzuri na wenye ufanisi kutoka kwa watu wote, ni muhimu kufanyika jitihada za uhamasishaji unaolenga kuelimisha Jamii ili kufahamu umuhimu wa zoezi la Sensa.

Kwa kutambua umuhimu huo, Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS) kwa kushirikiana na Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar (OCGS) imeandaa mkakati wa kuhamasisha na kuwashirikisha kikamilifu wananchi na wadau mbalimbali katika zoezi hilo.

Lengo kuu la uhamasishaji ni kuhakikisha wananchi wote wanaelewa umuhimu wa Sensa ili waweze kutoa ushirikiano na kushiriki katika zoezi zima la Sensa. Kwa upande mwingine ni kuhakikisha viongozi wa kisiasa na kijamii wanashiriki katika kuhamasisha umma kushiriki katika Sensa.

## 2. Maana ya Sensa ya Watu na Makazi

Sensa ya Watu na Makazi ni utaratibu wa kukusanya, kuchambua, kutathmini na kuchapisha au kusambaza takwimu za kidemografia, kiuchumi na kijamii kuhusiana na watu wote na makazi yao katika nchi kwa kipindi maalum. Kwa maana nyingine, Sensa ni zoezi maalum lenye lengo la kupata idadi ya watu wote katika nchi, kwa umri na jinsia, mahali wanapoishi, hali yao ya elimu, hali ya ajira, hali ya vizazi na vifo na hali ya makazi.

Kuwa na takwimu sahihi kuhusiana na watu ambazo zimechambuliwa na kuainishwa kwa makundi, ukubwa na mtawanyiko au msongomano wa watu na makazi katika maeneo yote ya nchi ni muhimu katika kupanga na kutekeleza mipango ya maendeleo ya kiuchumi na kijamii. Takwimu hizi za msingi ndizo zinazoweza kuainisha mahitaji halisi ya wananchi yakiwemo makundi yenye mahitaji maalum (kwa mfano, watu wenye ulemavu, nk) kwa kipindi cha sasa na kipindi kijacho, hivyo kurahisisha uandaaji wa sera na mipango ya maendeleo kulingana na mahitaji na mazingira yaliyopo.

Sensa za Watu na Makazi ambazo hufanyika katika nchi zote ulimwenguni, zilizoendelea na zinazoendelea, huendeshwa kwa kufuata kanuni, taratibu na miongozo maalum iliyokubalika kimataifa. Utaratibu unaofuatwa na nchi nyingi, Tanzania ikiwa

mojawapo, ni kufanya Sensa ya Watu na Makazi kila baada ya miaka kumi.

Kwa kawaida zoezi la Sensa hufanyika kwa kumtuma Karani wa Sensa (Mdadisi) kwenye eneo lililotengwa maalum kwa shughuli ya Sensa ili kuorodhesha idadi ya wanakaya wote waliolala katika eneo hilo siku ya Sensa pamoja na taarifa zao kulingana na maswali yaliyomo katika dodoso.

## 3. Sensa na Maendeleo

Maendeleo ya nchi yoyote hayana budi kulenga katika kuinua kiwango cha maisha ya wananchi wake. Mipango ya maendeleo ya nchi tangu uhuru imekuwa ikijikita katika kumkomboa Mtanzania kutokana na maadui ujinga, maradhi na umasikini. Kwa msingi huo, madhumuni makubwa ya Sensa ya mwaka 2012 ni kukusanya takwimu sahihi na za uhakika ili ziweze

kutumika kupima kiwango cha maendeleo kilichofikiwa pamoja na kuandaa miongozo itakayotumika katika kutayarisha mipango ya maendeleo ya muda mfupi na muda mrefu.

Takwimu zitakazokusanywa katika Sensa hiyo zitatumika katika kutunga sera za kiuchumi na kijamii na zitatumika pia kutathmini ubora wa hali ya maisha ya watu kwa ujumla. Hivyo, Sensa ya Watu na Makazi ya mwaka 2012, imeweka mkazo mkubwa katika maendeleo kwani serikali inatambua kuwa hatuwezi kupata maendeleo endelevu bila ya kuwa na takwimu sahihi na za kuaminika.

## 4. Umuhimu wa Sensa ya Watu na Makazi ya Mwaka 2012

Sensa ya Watu na Makazi ya mwaka 2012 ina umuhimu wa kipekee kwani mbali ya kutimiza malengo ya kawaida ya

Sensa, takwimu zitakazokusanywa katika Sensa hiyo zitatumika katika kutathmini utekelezaji wa mipango yetu mikubwa ya maendeleo ambayo imekuwa ikitekelezwa katika kipindi kilichopita. Mipango hiyo ni pamoja na Mkakati wa Kupunguza Umasikini na Kukuza Uchumi Tanzania - MKUKUTA kwa Tanzania Bara na Mkakati wa Kupunguza Umasikini Zanzibar - MKUZA kwa upande wa Zanzibar. Halikadhalika, takwimu za Sensa ya mwaka 2012 zitatumika kutathmini utekelezaji wa Malengo ya Milenia 2015.

## 5. Maandalizi ya Sensa ya Watu na Makazi ya Mwaka 2012

Utekelezaji wa zoezi la Sensa ya Watu na Makazi hufanyika katika hatua mbalimbali ambazo ni maandalizi, Sensa yenyewe na uchambuzi wa takwimu zilizokusanywa. Maandalizi ya Sensa ya Watu na Makazi 2012 yalianza toka mwaka 2004, ikiwa

ni kutenga maeneo ya kuhesabia watu, kutayarishaji na kupitia nyaraka muhimu za Sensa, kama vile madodoso, miongozo ya wasimamizi na makarani wa Sensa, fomu za kudhibiti ubora wa Sensa, kufanya Sensa ya Majaribio na Mpango wa Utoaji wa Takwimu.

## 5.1. Kutenga Maeneo ya Kuhesabia Watu

Ili kurahisisha kazi ya kuhesabu watu, nchi nzima imetengwa katika maeneo madogo madogo katika Mfumo wa Taarifa za Kijiografia yajulikanayo kama "Maeneo ya Kuhesabia Watu" Kila eneo lililotengwa limechorwa ramani inayoonyesha mahali eneo lilipo pamoja na mipaka yake. Ramani hizo ndizo zitakazotumika katika kuwaongoza Makarani wa Sensa (Wadadisi) wakati wa kuhesabu watu.



*Wataalamu wa kutenga maeneo wakiwa kazini kutenga maeneo.*

Utengaji wa maeneo ya kuhesabu watu umefanywa katika kila eneo la nchi ikiwa ni pamoja na maeneo ya makazi ya watu, visiwa, misitu, milima, maeneo yasiyo na makazi, mbuga za wanyama na kadhalika. Msingi wa hatua hii ya kutenga maeneo ni kuhakikisha kuwa kila mtu anayeishi nchini yumo ndani ya moja kati ya maeneo ya kuhesabia watu.

Lengo ni kuhakikisha kuwa kila atakayekuwepo ndani ya mipaka ya nchi yetu siku ya Sensa anahesabiwa na anahesabiwa mara moja tu. Hivyo basi, ni wajibu wa kila mwananchi kukumbuka kuwa anastahili kuhesabiwa mara moja na ni wajibu wa viongozi kusisitiza hilo wanapokutana na wananchi katika maeneo yao wakati wa shughuli mbalimbali.

## 5.2. Uhamasishaji

Uhamasishaji wa wananchi na wadau wengine kushiriki na katika kufanikisha Sensa ya Watu na Makazi ya mwaka 2012 umeanza muda mrefu. Kadri muda unavyokaribia siku ya Sensa ndivyo shughuli za uhamasishaji zitakavyoimarishwa na kuongezewa msukumo kwa lengo la kuhakikisha umma unatambua umuhimu wa Sensa

na kuunga mkono maandalizi na hatimaye kushiriki katika Sensa.

## 5.3. Sensa ya Majaribio

Katika kujiandaa na Sensa ya Watu na Makazi, ni kawaida kufanya Sensa ya Majaribio mwaka mmoja kabla ya Sensa yenyewe. Hivyo, ili kujiandaa vyema kwa ajili ya Sensa iliyopangwa kufanyika tarehe 26 Agosti 2012, Serikali ilifanya Sensa ya Majaribio ambayo ilianza tarehe 02 Oktoba 2011 na kumalizika ndani ya siku saba. Sensa hiyo ilifanyika katika maeneo 44 ya kuhesabiwa watu kwenye mikoa 11 (tisa Tanzania Bara na miwili ya Zanzibar). Mikoa hiyo ni Arusha, Dar es salaam, Kigoma, Kilimanjaro, Manyara, Mara, Mtwara, Njombe, Pwani, Mjini Magharibi na Kaskazini Pemba.



*Mwezeshaji akiwa na Wasimamizi na Makarani wa Sensa ya Majaribio katika mafunzo.*

Katika Sensa hiyo, kaya 4,173 zenye jumla ya watu 19,876 zilishiriki. Miongoni mwao 10,276 walikuwa wanawake na 9,600 walikuwa wanaume. Matokeo yanaonesha kuwa Karani wa Sensa alitumia wastani wa dakika 30 kukamilisha mahojiano katika kaya moja kwa kutumia Dodoso Fupi na dakika 36 kwa Dodoso Refu.



*Karani wa Sensa akichukua maelezo ya kaya wakati wa Sensa ya Majaribio*

Kwa ujumla Sensa ya Majaribio ilifanyika kwa mafanikio kwani iliweza kufikia malengo yaliyotarajiwa. Sensa hiyo ililenga katika kutathmini kwa ujumla maandalizi ya Sensa ya Watu na Makazi mwaka 2012 ikiwa ni pamoja na kupima usahihi wa vifaa, nyaraka na kumbukumbu mbalimbali

zitakazotumika, yakiwemo madodoso, miongozo na fomu za kudhibiti ubora wa Sensa. Aidha, Sensa ya Majaribio ililenga kupima kwa kiasi gani mfumo wa Serikali umejiandaa kufanya Sensa hiyo na kwa jinsi gani wananchi na jamii nzima inavyoitikia wito wa kushiriki Sensa.

### 5.4. Maandalizi Mengine

Maadalizi mengine yanahusu ununuzi, usafirishaji na usambazaji wa vifaa vya Sensa. Shughuli hii inafanywa kwa tahadhari kubwa na wataalamu wetu kwa kuzingatia sheria ya manunuzi, ubora wa vifaa, muda wa kuwasilishwa na kusambazwa mapema kabla ya siku ya Sensa.

## 6. Kamati za Sensa

Serikali imeunda Kamati za Sensa kuanzia ngazi ya Taifa hadi Wilaya. Katika ngazi

ya Taifa kuna Kamati Kuu ya Sensa inayoongozwa kwa pamoja na Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Makamu wa Pili wa Rais wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar.

Nyingine ni Kamati ya Ushauri, Kamati ya Wataalamu na Kamati ya Wadau.

Katika ngazi ya Mkoa na Wilaya kuna Kamati ambazo zinaongozwa na wakuu wa Mikoa na Wilaya husika. Kamati hizi zina kazi za kusimamia zoezi la Sensa katika maeneo yao, kutoa ushauri wa utekelezaji na kuuandaa umma kwa kuwaelimisha wananchi juu ya Sensa pamoja na matarajio ya ushiriki wao katika zoezi hili muhimu kwa taifa.

## 7. Wajibu wa Viongozi

Viongozi wote wa Serikali Kuu, Serikali

za Mitaa na Vijiji jukumu lao kubwa katika Sensa ni kuhakikisha kuwa Sensa inafanyika kwa mafanikio makubwa. Hili litawezekana endapo tu viongozi watakuwa mstari wa mbele katika kuelimisha wananchi wajibu wao na nini cha kufanya wakati wa Sensa. Lengo letu ni kuendeleza sifa yetu ya kufanya Sensa zenye mafanikio na mfano wa kuigwa barani Afrika.

Wajibu wa kwanza wa viongozi ni kuuandaa umma kwa kuuelimisha, kuuhamasisha na kuwashajiisha wananchi kuhusu umuhimu wa Sensa ili waweze kushiriki pamoja na kutoa ushirikiano na msaada unapohitajika wakati wote wa Sensa. Kazi hii itafanyika kwa njia za vikao mbalimbali, semina, mikutano ya hadhara na pia kwa njia nyinginezo za maandishi, vielelezo, mabango pamoja na kushirikisha vyombo vya habari, kama vile, redio, televisheni,

magazeti na kwa njia ya mtandao wa intaneti.

Kwa upande mwingine, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imemteua Kamishna wa Sensa. Aidha Serikali ya Mapinduzi Zanzibar imemteua Kamisaa wa Sensa kwa Zanzibar. Majukumu makubwa ya viongozi hao ni pamoja na:-

- Kuhamasisha viongozi, wadau wa maendeleo na umma kwa ujumla juu ya umuhimu wa Sensa ya Watu na Makazi ya mwaka 2012, pamoja na ushiriki wa kila mmoja katika zoezi hili wakati wa kuhesabu watu na wakati wa kutoa matokeo ya Sensa.

- Kuwa kiungo kati ya Ofisi ya Taifa ya Takwimu, Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar na viongozi wa ngazi mbalimbali za Serikali na wale wa Kisiasa na Kijamii katika

utekelezaji wa shughuli mbalimbali za Sensa.

- Kuunganishanakuimarishaushirikiano miongoni mwa vyombo mbalimbali vya habari katika kulitangaza zoezi la Sensa ya mwaka 2012 kupitia mikutano, mijadala/mahojiano na makala katika vyombo hivyo.

Halikadhalika, viongozi wa Serikali za mitaa watashirikishwa na kupewa majukumu ya kuwaongoza Makarani wa Sensa pamoja na wasimamizi wao katika maeneo yao wakati wa zoezi zima la Sensa. Viongozi hawa ndiyo watakuwa mihili na wenyeji wa makarani na maafisa wa Sensa katika maeneo ya kuhesabia watu. Hivyo, ni wajibu wao pia kuhakikisha kuwa wananchi katika maeneo yao wanahesabiwa na wanahesabiwa mara moja tu.

Viongozi wa dini pia, wanayo nafasi muhimu katika kuuandaa umma kwa kushiriki kikamilifu katika kutoa elimu ya Sensa na kutoa wito kwa waumini wa dini zao kujiandaa na kushiriki katika Sensa.

Sambamba na kuwatumia viongozi hao, uhamasishaji utafanyika kwa kuwashirikisha wanafunzi mashuleni, vyuoni vikundi vya sanaa na burudani ambavyo vitahamasishwa ili viweze kutumia fani za sanaa kama nyimbo, kwaya, michezo ya kuigiza, ngonjera, ngoma za utamaduni, n.k. katika kutoa elimu ya Sensa.

## 8. Wajibu wa Wananchi

Mwananchi ndiye mlengwa mkuu wa Sensa hivyo ni wajibu wake kutambua umuhimu wa kushiriki zoezi hili na kufanikisha malengo na madhumuni ya Sensa kama yalivyoelezwa. Kwa hiyo, wajibu mkubwa

wa mwananchi ni kuhakikisha kuwa anajiandaa kuhesabiwa kwa kuelewa siku ya Sensa yenyewe na kujibu kwa usahihi na kwa makini maswali atakayoulizwa na Karani wa Sensa. Kwa kufanya hivyo, malengo ya Sensa yatatimizwa kama yanavyotarajiwa.

## 9. Maswali ya Sensa

Kutakuwa na aina tatu za madodoso katika Sensa ya Watu na Makazi ya mwaka 2012 ambayo yatakuwa na maswali kulingana na aina ya taarifa/takwimu zinazotakiwa kukusanywa. Kutakuwa na **Dodoso Fupi, Dodoso Refu** na **Dodoso la Jamii.** Mahali ambapo Dodoso Fupi litatumika kuhesabu watu, Dodoso Refu halitatumika na pale ambapo Dodoso Refu litatumika Dodoso Fupi halitatumika.

Sehemu kubwa ya nchi (asilimia 70), Dodoso Fupi ndilo litakalotumika

kuhesabu watu. Maeneo yaliyobaki (asilimia 30) yatakayochaguliwa kwa kuzingatia utaalam wa kukokotoa sampuli litatumika Dodoso Refu.

Maswali ya **Dodoso Fupi** yamo pia katika Dodoso Refu hivyo maswali hayo yatajibiwa na watu popote pale ambapo madodoso haya yatatumika. Maswali hayo yatauliza kuhusu jina la mkuu wa kaya; pili, majina ya watu wote waliolala katika kaya hiyo katika usiku wa kuamkia tarehe 26 Agosti, 2012; na tatu, uhusiano wa watu hao na mkuu wa kaya. Uhusiano huo unaweza kuwa ni mme, mke, mtoto, baba, mama mzazi, mjukuu, ndugu au rafiki. Maswali mengine yatakayofuata yatataka kujua jinsi, umri, ulemavu, hali ya ndoa, uraia, mahali anapoishi na anaposhinda mwanakaya. Aidha, maswali juu ya vifo na vifo vitokanavyo na uzazi

katika kaya, na Watanzania wanaoishi nje ya nchi yataulizwa.

Kwa wale watakaoulizwa maswali kutoka **Dodoso Refu** watatakiwa kujibu maswali ya ziada ambayo yatahusu:- taarifa binafsi za watu wote; elimu kwa watu walio na umri wa miaka minne na zaidi; shughuli za kiuchumi zikiwemo aina ya mazao yanayolimwa na ufugaji wa mifugo na samaki kwa watu walio na umri wa miaka mitano na zaidi. Aidha, maswali yanayohusu nyumba na umiliki wa vifaa yataulizwa. Vile vile wanawake wenye umri wa miaka 12 na zaidi wataulizwa maswali yanayohusu uzazi.

Maswali yote haya yana lengo la kukidhi mahitaji ya takwimu mbalimbali ambayo Taifa linahitaji hivi sasa na baadaye kwa ajili ya upangaji na utekelezaji mzuri wa

mipango mbalimbali ya maendeleo. Hivyo, mkuu wa kaya anaombwa sana ayaelewe na ayazingatie maswali yote haya ili aweze kuyajibu kwa ufasaha.

Inawezekana katika usiku wa kuamkia siku ya Sensa, mgeni alilala katika kaya na kesho yake akawa ameondoka. Kwa utaratibu wa Sensa, mgeni huyo atatakiwa kuhesabiwa hapo katika kaya aliyolala na siyo huko atakakokutwa baada ya Siku ya Sensa. Kwa ajili hiyo, ni vizuri kwa mkuu wa kaya akapata majibu ya maswali yanayohusu mgeni wake hasa yale yanayohusu kazi na elimu, kabla mgeni huyo hajaondoka ili aweze kuyajibu maswali ya Sensa kwa niaba ya mgeni wake.

**Dodoso la Jamii** litakalojazwa ndani ya siku 3 kabla ya siku ya Sensa, wakati Karani

akiwa analitambua eneo lake la kuhesabia watu, litakusanya taarifa zinazohusiana na huduma za jamii kama vile shule, vyoo, hospitali, vituo vya afya, zahanati, masoko, huduma za fedha, majosho, vyanzo vya maji, miundombinu na mazingira pamoja na matukio yaliyotokea katika kipindi cha mwaka mmoja uliopita ambayo ni kero kwa jamii husika katika eneo la kuhesabia watu.

Viongozi wa jamii husika, walimu, n.k. watahusika kujibu maswali ya dodoso hili kwa vile wana uelewa wa kutosha wa eneo hilo pamoja na huduma zinazopatikana ndani yake.



*Wataalamu wa Ofisi ya Taifa ya Takwimu wakitoa maelezo kwa baadhi ya viongozi wa Ofisi hiyo kuhusu maswali mbali mbali yatakayoulizwa wakati wa Sensa ya Watu na Makazi.*

## 10. Sheria ya Takwimu na Usiri wa Taarifa za Wanakaya

Sensa ya Watu na Makazi ya mwaka 2012 inafanyika kwa mujibu wa Sheria ya Takwimu Na. 1 ya mwaka 2002.

Kutokana na sheria hiyo taarifa zote binafsi za watu zitakazokusanywa wakati wa Sensa ni SIRI na zitatumika kwa madhumuni ya kitakwimu tu. Kwa hiyo, watu wote watakaohusika na kazi ya kuhesabu watu watalazimika kula kiapo cha kutunza siri juu ya taarifa binafsi za watu watakaowahesabu kabla ya kuanza kazi hiyo. Kwa yule atakayekiuka sheria hiyo atachukuliwa hatua zinazostahili kisheria.

## 11. Maeneo Maalum ya Kuhesabu Watu

Mbali na maeneo ya kuhesabia watu yaliyoainishwa, pia yapo maeneo ambayo ni tofauti na hayo lakini yatakuwa na watu ambao, kwa mujibu wa taratibu za Sensa itabidi na wao wahesabiwe.

Maeneo hayo ni pamoja na hospitali, vyuo, shule, kambi za jeshi, kambi za

wakimbizi, nyumba za kulala wageni, magereza na mengine kama hayo.

Wote watakaokuwa katika maeneo hayo katika usiku wa Sensa watapitiwa na Karani wa Sensa kuhesabiwa. Ombi kwa watu hawa ni kuwa iwapo asubuhi ya mkesha wa siku ya Sensa wataondoka katika maeneo hayo, kwa mfano iwapo walikuwa wamelazwa hospitalini na kurejea majumbani mwao, wasikubali kuhesabiwa tena huko walikokwenda kwa vile hesabu yao itakuwa imechukuliwa pale walipolala.

## 12. Wawindaji, Wavuvi na Wachungaji

Katika jitihada za kuhakikisha kuwa kila mtu anahesabiwa na anahesabiwa mara moja tu, kuna makundi mbalimbali ya watu ambayo yatatakiwa kuhamasishwa ili yatoe ushirikiano mzuri katika

kufanikisha kazi ya kuhesabu makundi hayo.

Makundi hayo ni yale ya wawindaji, wavuvi, wachungaji wanaohama hama, watafutaji madini, na baadhi ya wakulima ambao wana mashamba yaliyo mbali na makazi yao ya kawaida. Itakuwa sio rahisi kwa Karani wa Sensa kuelewa ni wapi walipo ili kuweza kufuatwa huko na kuhesabiwa. Kwa ajili hiyo watu hawa watatakiwa kurudi kwenye makazi au makambi yao ya kawaida ili waweze kuhesabiwa siku ya Sensa.

## 13. Wasafiri

Kundi jingine la watu ambao ushirikiano wao utahitajika sana wakati wa Sensa ni wasafiri. Kundi hili ni la watu ambao watakuwa safarini usiku wa kuamkia siku ya Sensa, yaani watakuwa katika

vyombo vya usafiri kama garimoshi, mabasi, ndege, meli (na vyombo vingine vya usafiri wa baharini). Watu hawa watahesabiwa pale watakapoanza safari au watakapomalizia safari zao.Ili kufanikisha zoezi la kuwahesabu watu wa kundi hili utaratibu umeandaliwa wa kuwaweka Makarani wa Sensa katika vituo vya usafiri, yaani vituo vya garimoshi, mabasi, viwanja vya ndege, bandari zote na kuhakikisha kuwa wasafiri wote wanahesabiwa kabla ya kuondoka usiku huo, au wanahesabiwa mara baada ya kuwasili katika vituo wanapoteremkia. Katika kuhakikisha wasafiri hawahesabiwi zaidi ya mara moja, kila msafiri baada ya kuhesabiwa atapewa kadi maalum itakayoonyesha kuwa tayari amehesabiwa.

Iwapo msafiri ataanza safari kabla ya usiku wa Sensa na kuwasili kesho yake au baadaye, basi ahakikishe anahesabiwa katika kituo cha kuteremkia na iwapo wamehesabiwa kabla ya kuondoka, aepukane na kuhesabiwa mara ya pili huko atakakoishia. Ikiwa ataondoka baada ya kulala katika kaya yake lakini kabla ya Karani wa Sensa hajapita, asihesabiwe huko anakoteremkia kwani atahesabiwa katika kaya alimokuwa amelala katika usiku huo wa Sensa.

## 14. Watu Wasiokuwa na Makazi Maalum

Watu hawa ni wale ambao hawana nyumba za kuishi hivyo hawawezi kuhesabiwa kwenye kaya yoyote ile. Wao hulala sehemu mbalimbali kwa mfano katika maeneo ya wazi, sokoni, barazani, kwenye vituo vya garimoshi na vya mabasi, bandarini na sehemu

nyingine. Watu hawa pia wanapaswa kuhesabiwa, hivyo utaratibu maalum umewekwa kuhakikisha kuwa watu hao wanahesabiwa pia usiku wa kuamkia siku ya Sensa mahali Karani wa Sensa atakapowakuta wamelala.

## 15. Siku ya Sensa

Siku ya Sensa imepangwa kuwa ni usiku wa Jumamosi ya tarehe 25 Agosti kuamkia siku ya Jumapili, tarehe 26 Agosti, 2012. Hivyo watu wote waliolala katika kaya usiku wa kuamkia siku ya Sensa watahesabiwa.

## 16. Muda wa Kuhesabu

Kwa kawaida kazi ya kuhesabu watu inatakiwa ifanyike kwa siku moja tu. Hata hivyo, kutokana na ukubwa wa kazi na hali halisi ya nchi yetu, kuna uwezekano mkubwa kazi hiyo kuchukua zaidi ya

siku moja. Kwa kuzingatia hali hii, kazi kuhesabu watu impengwa kukamilika ndani ya siku saba. Shabaha ya kuweka muda maalum wa kuhesabu watu ni kuondoa uwezekano wa kusahau watu na taarifa zao, waliolala katika kaya zao usiku wa kuamkia Sensa na kuondoka kabla ya Karani wa Sensa kufika na kuhesabu watu katika kaya husika.

**SENSA KWA MAENDELEO**
**JIANDAE KUHESABIWA**